TANGAZO LA SERIKALI NA. 402 la tarehe 24/5/2024

SHERIA YA USIMANIZI NA USHURU WA BIDHAA,

(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 128(2))*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA GARI MOJA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA AFYA ENDELEVU CHINI YA TAASISI YA BENJAMIN WILLIAM MKAPA YA MWAKA 2024

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Gari Moja kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Afya Endelevu Chini ya Taasisi ya Benjamin William Mkapa ya Mwaka 2024, na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 08 Aprili, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa na Taasisi ya Benjamin William Mkapa Foundation kwa gari moja lililoanishwa katika Jedwali la Amri hii, lililoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi kabla ya kibali kupitia forodha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Afya Endelevu, unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa gari tajwa-

(a) litahamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii; au

(b) litatumika kwa matumizi mengine mbali na yaliyoainishwa katika Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itakoma kutumika tarehe 05 mwezi Oktoba, 2024.

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na | Maelezo | Namba ya Chesesi | Namba ya injini | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA LANDCRUISER PRADO 2.8 1GD TXL, GDJ150R-GKTEY SFX: U2, 7-Seater, Year of Manufacture:2023 | JTEBR3FJ10-K322503 | 1GD-9210299 | 01 |

Dodoma,
13 Mei, 2024.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*